

Kwa nini tunanakili matukio?

Tunataka kuweka wazi matukio ya ubaguzi na hali halisi ya maisha mjini Berlin, na kurekodi Mienendo na shughuli za mrengo wa kulia. Matokeo ya ripoti hii yatawasilishwa kwa wanasiasa wa eneo hilo, wakazi na watu waliojitolea katika wilaya. Kisha wanaweza kujibu kwa kuchukua hatua za kisiasa.

Kwa hivyo unaombwa kuwasilisha ripoti yako ya yale uliopitia na yale ulio yaona kwetu kupitia:

Barua pepe: info@berliner-register.de

Simu: +49 (0)1520 4425746 (Kati Becker)

Twitter: @RegisterBerlin

Wavuti: www.berliner-register.de

Programu: www.berlin.de/andi

Almashauri ya Nakala za Berlin

Rejesta za Berlin hunakili matukio katika vitongoji vyake ambapo watu wametengwa ki jamii. Tunachapisha matukio haya katika nakala yetu maalum na kuyatathmini kila mwaka. Nakala hii maalum inaweza kupatikana kwenye tovuti yetu ifuatayo: www.berliner-register.de/chronik

In Trägerschaft von:



Gefördert durch das Landesprogramm „Demokratie. Vielfalt. Respekt. Gegen Rechtsextremismus, Rassismus und Antisemitismus“ der Senatsverwaltung für Justiz, Vielfalt und Antidiskriminierung.



V.i.S.d.P.: A. Wächter, pad gGmbH,
Kastanienallee 55, 12627 Berlin



Tunanakili nini?

Tunaweka kila tukio kwa kategoria ya maudhui na aina ya tukio.

Uainishaji wa maudhui

- **Ubaguzi wa rangi**
kwa watu weusi, watu wanaotambulika kuwa Waislamu, Romn*ja na Sinti*zze, watu wanaotambulika kutoka kwa bara la Asia na wengineo.
- **chuki dhidi ya Wayahudi**
- **Uadui dhidi ya watu wa LGBTIQ***
Ufupisho wa: Wasagaji, Mashoga, Mwenye jinsia mbili, Trans, Intersex na Queer.
- **Uadui dhidi ya watu wasio na makaazi**
- **Uhasama dhidi ya watu wenye ulemavu (Ableism)**
- **Kupunguza/kutukuza Ujamaa wa Kitaifa**
- **Kujitangaza kwa mrengo wa kulia**
Matangazo ya vikundi vya mrengo wa kulia vilivyokithiri au shughuli za kampeni za uchaguzi
- **Wapinzani wa kisiasa (wa kulia uliokithiri)**
- **Kupinga ufeministi (kama mkakati wa kisiasa)**

Aina za matukio

- **Vitisho, matusi, na lugha chafu**
- **Mashambulizi** k.m. mashambulizi ya kimwili, mashambulizi ya moto
- **Ubaguzi wa kimuundo** k.m. ubaguzi wa walio mamlakani, taasisi au wasifu wa rangi
- **Propaganda** k.m. stika na graffiti
- **Matukio k.m.** k.m. maandamano, meza za habari, hafla za ukumbini
- **Uharibifu wa mali** k.m. mabango ya ukumbusho, mawe ya kikwazo
- **BVV** k.m. hoja na hotuba za kibaguzi katika vikao vya hal-mashauri ya wilaya
- **Matukio mengine**

